

OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA LIWALE.

KIBUTUKA SEKONDARI,  
S.L.P 195, LIWALE  
TAREHE .....

MOB: 0714257078 / 0777388733

KUMB.NA.ED/KSS/VOL.I/17

JINA LA MWANAFUNZI: .....

LIWALE

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KIBUTUKA ILIYOPO WILAYA YA LIWALE MKOA WA LINDI MWAKA 2021**

**1. UTANGULIZI**

Ninafurahi kukujulisha kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha I mwaka **2021** Shule Ya Sekondari Kibutuka. Shule itafunguliwa tarehe 11/ 01 / **2021**. wewe unatakiwa kuripoti hapa shuleni tarehe 11/ 01/ **2021** bila kukosa. Shule ya sekondari kibutuka ipo kusini mwa mji wa liwale **km 64 (mile 40)**, Kutoka liwale mjini kwenye barabara ya Nachingwea-Liwale Ipo katika kijiji cha Kibutuka, umbali wa mita **200** kutoka kibutuka kuelekea njia inyoelekea katika kijiji cha Ngumbu.

**2. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA  
(A) SARE ZA SHULE**

WASICHANA

1. Sketi 2 rangi ya kaki (SKETI IVUKE MAGOTI) MSHONO IWE RINDA BOX.
2. Mashati 2 meupe mikono mifupi tetroni
3. Viatu vyeusi vya ngozi vya kutumbukiza, vya kufunga kwa kamba au Gidamu, visiwe na visigino virefu kwa ajili ya darasani.
4. Soksi nyeupe/ Jozi 2 au Zaidi.
5. Tai rangi ya kaki sawa na sketi.
6. Sketi 2 Bluu (tetroni) kwa ajili ya kazi za nje.
7. Tracksout nyekundu kwa ajili ya michezo

8. Viatu cha raba rangi yeyote kwa ajili ya michezo.
9. Fulana 2 njano zinapatikana shule picha kwa ajili ya kazi za nje michezo.
10. Hijabu nyeupe inaruhusiwa kwa anayetaka tu, ila siyo lazima, itavaliwa na sare ya shule, **MITANDIO HAIRUISIWI.**

#### WAVULANA

1. Suruali 2 za rangi ya kaki (Tetroni) upana wa suruali chini usipungue 18.  
**MODO HAZITAKIWI.**
2. Mashati 2 meupe mikono mifupi tetroni.
3. Soksi nyeupe / Nyeusi Jozi 2 au Zaidi.
4. Tai rangi ya Suruali (Kaki).
5. Kaptura 2 bluu (tetroni) kwa ajili ya michezo na kazi za nje.
6. Viatu vyeusi vya ngozi vya kutumbukiza, vya kufunga kwa kamba au Gidamu, visiwe na visigino virefu kwa ajili ya darasani.
7. Mkanda mweusi uvaliwe na suruali.
8. Tracksout nyekundu kwa ajili ya michezo
9. Viatu cha raba rangi yeyote kwa ajili ya michezo.
10. Fulana 2 njano isiwe na maandishi / picha kwa ajili ya kazi za nje michezo.

#### (B) VIFAA VYA MASOMO DARASANI NA NJE

*( Ni Muhimu Kwa Kila Mwanafunzi Akaja Navyo)*

- i. Madaftari 10 au Zaidi makubwa (itafaa Zaidi counter book)
- ii. Kalamu (peni na penseli ) za kutosha
- iii. Mkebe wa hesabu na rula
- iv. Dictionary
- v. Rim 1 ( bunda la karatasi nyeupe )
- vi. Jembe (lililowekewa mpini ) kwa ajili ya kilimo na usafi wa mazingira.
- vii. Slasher (fyekeo) 1

#### (C) WANAFUNZI WA HOSTELI

Wanafunzi wanaotoka mbali na shule wanatakiwa kukaa hosteli, shule itawezesha chumba na kitanda.

- i. Mzazi atampatia chakula mtoto wake, milo mitatu kwa kutwa cha nusu muhula au muhula mzima ili kuepuka mwanafunzi kukatisha masomo kufuata chakula nyumbani. *(wasiliana na mkuu wa shule ili akujulishe kiasi cha kuchangia chakula 0714257078 / 0713493911 )*.
- ii. Mzazi atamwezesha mtoto wake nauli ya kutoka na kurudi likizo.
- iii. Mzazi atamwezesha mtoto wake sabuni, mafuta ya kupaka na matibabu.
- iv. Mzazi atamwezesha mtoto wake godoro la kulalia ft  $2 \frac{1}{2} \times 6$  .

## (D) WANAFUNZI WA KUTWA

Wazazi watachangia chakula cha mchana cha wanafunzi (watoto wao) ili wasisome wakiwa na njaa.

### 3. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu Na. 25 ya Mwaka 1978 na kama ilivyorekebisha kwa sharia Na. 10 ya Mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya Elimu, sayansi, teknolojia an ufundi, yenye dhamana ya Elimu nchini na Ofisi ya RAIS-TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

1. Heshima kwa viongozi, wazazi na wafanyakazi wote.
2. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
3. Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation).
4. Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
5. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya juu kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
6. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
7. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
8. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
9. Kutunza mali za umma. ( Mwanafunzi akiharibu kiti au meza atalipa )

3.2.Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kusimamishwa au kufukuzwa shule.

- a) Wizi
  - b) Uasherati na ushoga
  - c) Ubakaji
  - d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevyia
  - e) Kupiga au kupigana
  - f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
  - g) Kudharau bendera ya taifa
  - h) Kupata au kusababisha mimba
  - i) Kuoja au kuolewa
  - j) Kutoa mimba
  - k) Kukataa adhabu kwa makusudi
  - l) Kuwa na au kumiliki simu ya mkononi
4. Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi.
- a) “Medical examination form” ambayo itajazwa na mganga mkuu wa hospitali ya serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni.

- b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
  - c) Fumu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.
5. Tafadhali soma kwa makini maelezo / maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

.....

MKUU WA SHULE.

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA  
REGION ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT  
STUDENT MEDICAL EXAMINATION CERTIFICATE

(To be completed by government medical officer and returned to the headmaster of kikutuka s.s)

The head master  
Kikutuka secondary school  
p.o.box 195 liwale

to the medical officer

\_\_\_\_\_

\_\_\_\_\_

Ref: \_\_\_\_\_

please examination the student mentioned above and examination on his / her health by responding to the following items. Kindly put a tick or cross in front of either YES or NO as you find appropriate.

-----  
HEADMASTER.

NO

YES

- a) Eye (sight)?  
If yes, state .....
  - b) Hearing?  
If yes, state .....
  - c) Speech?  
If yes, state .....
  - d) T.B?  
If yes, state .....
  - e) Blood Pressure?  
If yes, state .....
  - f) Allergy?  
If yes, state .....
  - g) Any Physical Disability?  
If Yes state .....
  - Do you, therefore, recommend the said student medically fit for studentship at this school?  
No / Yes if no please, state reasons.
  - h) UPT.....  
.....
- Date ..... Name and Signature of MO .....  
Designation & stamp .....

(A) TAMKO LA MWANAFUNZI KUKUBALI NAFASI NA MKATABA

Mimi ..... (jina) wa  
.....(mahali) nakubali kujiunga kidato cha .....  
Katika shule ya sekondari kikutuka na nitafuata sheria zote na kanuni za shule na  
sitashiriki katika migomo, fujo, utoro na makosa ya jinai. Ninakubali kuadhibiwa pale  
itakapostahili.

SAHIHI ..... TAREHE .....

(B) TAMKO LA MZAZI / MLEZI KUKUBALI WAJIBU WA KUSOMESHA

Mimi ..... (jina) wa  
.....(mahali) ambaye ni mzazi / mlezi wa  
..... (jina la mwanafunzi). Ninakubali  
wajibu wa kutekeleza majukumu yanayonihsu mimi mzazi/ mlezi ya kumgharamia  
mwanafunzi mtajwa katika masomo yake. Ninakubaliana na sheria na kanuni na  
maelezo mengine yaliyotolewa na yatakayotolewa na shule.

SAHIHI ..... TAREHE .....